

**MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI (VETA)  
CHUO CHA UFUNDI STADI - VETA ULYANKULU  
MKATABA WA ZABUNI**

Na. ya Mkataba: VETA/ULY/UV20/22/23

Mkataba huu umesainiwa leo tarehe 28 Januari, 2022

**KATI YA**

Chuo cha Ufundi Stadi Veta Ulyankulu S.L.P. 111 Ulyankulu ambacho kinaiwakilisha Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, S.L.P 802 Dodoma (ambacho katika Mkataba huu atajulikana kama "Mwajiri") kwa upande mmoja;

**NA**

**M/S UNIQUE OFFICE SOLUTION & GENERAL SUPPLY** (ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama "Mzabuni") kwa upande mwingine

**KWA KUWA** Mwajiri ana mpango wa kujenga Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya Uvinza.

**KWA KUWA** Mwajiri anatumia rasilimali zake za ndani kwa ushirikiano na rasilimali za nje kwa ajili ya Ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya Uvinza;

**KWA KUWA** Mwajiri amefanya majadiliano na Mzabuni kwa ajili ya kuleta Vifaa vya Ujenzi

**NA KWA KUWA** Mwajiri amempatia Mzabuni Mchanganuo wa Vifaa vya Ujenzi unaonyesha Vifaa vinavyotakiwa kuletwa;

**HIVYO BASI, PANDE ZOTE MBILI ZINAKUBALIANA KAMA IFUATAVYO:**

**1. GHARAMA YA ZABUNI**

Kwamba, kwa gharama ya Shilingi za Tanzania 18,610,000/= (Millioni Kumi na Nane Laki Sita Kumi Eifu Tu) Mzabuni atafanya kazi hiyo kwa masharti yaliyo katika Mkataba huu.

NA.	AINA YA KAZI	KIASI	MAELEZO
1.	VIFAA VYA UJENZI	3,940,000	
2.	VIFAA VYA UJENZI	3,125,000	
3.	VIFAA VYA UJENZI	11,545,000	
	<b>JUMLA KUU</b>	<b>18,610,000</b>	

Katika Mkataba huu, kiasi hiki cha Fedha kitajulikana kama "Gharama ya Vifaa vya Ujenzi"

**2. NAMNA YA KUFANYA MALIPO**

Mwajiri atamlipa Mzabuni kwa Hundi ndani ya Siku Saba (07) mara baada ya kuleta mzigo

**3. MAMBO YALIYO NJE YA UWEZO WA KIBINADAMU**

Itakapotokea jambo lolote lililo nje ya uwezo wa kibinadamu kama vile mafuriko, kimbunga, tetemeko la ardhi na mambo yanayofanana na hayo, pande zote mbili zitapata nafasi ya kulijadili na kulipatia ufumbuzi wa haraka.

**4. NOTISI (NOTICES)**

Mawasiliano yote, Hati, Notisi yatakayofanyika katika Mkataba huu, yatafanyika kwa ama kupelekwa moja kwa moja (physically) kwa upande wowote wa Mkataba au kupitia anwani ya Posta kwa barua iliyosajiliwa (registered mail).

**5. SHERIA ZINAZOTUMIKA**

Sheria za kutafsiri Mkataba huu na ufanyaji wa kazi katika Mkataba huu ni Sheria za Tanzania.

## 6. RUSHWA

Iwapo Mzabuni au Wasaidizi wake katika kutekeleza Zabuni hii watajihusisha na masuala yoyote ya Rushwa ama Jinai yoyote, basi Mwajiri anaweza kuvunja Mkataba huu.

## 7. KUVUNJWA KWA MKATABA

Mkataba huu unaweza kuvunjwa na upande wowote wa Mkataba huu.

### (a) Mkataba kuvunjwa na Mwajiri:

Bila ya kuathiri haki zozote za Mwajiri, iwapo Mzabuni akifanya makosa yafuatayo:

- i. Kuchelewa kuleta Vifaa kwa wakati bila ya sababu yoyote ya msingi, au
- ii. Kutofuata maelekezo ya Mwajiri wakati wa uletaji wa Vifaa
- iii. Mzabuni akimpa Mtu mwingine kazi ya kuleta Vifaa bila ya kupata idhini ya Mwajiri

## 8. USIRI

Nyaraka zote zitakazokuwa zimetumika katika Zabuni inayohusiana na Mkataba huu hazitatumika kwa madhumuni mengine yoyote isipokuwa kwa Zabuni inayohusu Mkataba huu. Pia taarifa yoyote itakayopatikana wakati wa Zabuni hii haitatumika kwa madhumuni mengine yoyote isipokuwa kwa Zabuni inayohusu Mkataba huu.

## 9. USULUHISHI WA MIGOGORO

Mgogoro wowote utakaotokana na utekelezwaji wa Mkataba huu au baada ya utekelezwaji wa Mkataba utasuluhishwa kwa majadiliano ya pande zote za Mkataba. Iwapo majadiliano yatashindwa kusuluhisha mgogoro, basi upande wowote utatoa Notisi ya siku kumi na nne ya kupeleka mgogoro usuluhishi kwa njia ya usuluhishi (arbitration).


IMESAINIWA NA KUWEKWA MHURI, KWA NIABA YA MAMLAKA YA ELIMU  
NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI, NA CHUO CHA UFUNDI STADI CHA  
VETA ULYANKULU

Jina: RICHARD MZAMBWA Saini: 

Wadhifa: Mkuu wa Chuo Tarehe: 28/01/2022



Mbele ya (Shahidi)

PRINCIPAL VTC ULYANKULU  
P.O. Box III  
ULYANKULU

Jina: JAVAN MAHWIKIZI Saini: 


Wadhifa: M/KITI KAMATI UTAZI Tarehe: 28/01/2022

IMESAINIWA NA MZABUNI

Jina:  Saini: 

Wadhifa: Mkung'eni Tarehe: 28/1/2022

Mbele ya (Shahidi)

Jina: Happiness Enock Saini: 

Wadhifa: Cashier Tarehe: 28.1.2022